



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

BODI YA KAHAWA TANZANIA



TANGAZO

UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2026/2027

UTANGULIZI

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anawatangazia wadau wote wa kahawa tarehe za ufunguzi wa msimu mpya wa masoko ya kahawa kwa mwaka 2026/2027. Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 (1) ya Kanuni za Kahawa 2013. Tarehe za ufunguzi wa msimu na kuanza kwa ununuzi wa kahawa katika kanda za uzalishaji kahawa ni kama ifuatavyo;

Na.	Kanda	Mkoa	Tarehe ya Ufunguzi
1.	Kigoma	Kigoma, Katavi	30 April, 2026
2.	Mara	Mara, Mwanza	30 Aprili, 2026
3.	Kagera	Kagera	1 Mei, 2026
4.	Mbeya, Songwe	Mbeya, Songwe	15 Juni, 2026
5.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 Julai, 2026
6.	Kaskazini	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 Julai, 2026

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MSIMU HUU 2026/2027

1. Katika kanda zote za ukusanyaji na uuzaji wa kahawa kwa wakulima wadogo utaendelea kufanyika kupitia AMCOS zilizopo katika maeneo yao. Aidha vyama vikuu vya ushirika vitakuwa na wajibu wa kuratibu taarifa za makusanyo na utoaji wa huduma nyingine zitakazo kubaliwa
2. Bodi inashauri Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa kutoa vibali vya kununua kahawa kwa wanunuzi wenye nia ya kununua kahawa kwenye Halmashauri zao mapema kabla ya tarehe ya kuanza msimu ikiwa ni moja ya masharti yaliyotolewa ili kupata leseni ya ununuzi wa kahawa kwa mujibu wa Jedwali la Tatu la Kanuni za Kahawa 2013. Endapo Halmashauri itachelewesha au kukataa kutoa kibali pasipo sababu za msingi, Bodi itatoa leseni kwa mujibu wa Kanuni ya 26 (2) ya Kanuni za Kahawa, 2013.
3. Maombi ya leseni zote mpya na maombi ya kuhuisha (renewal) leseni kwa wanunuzi wa kahawa yatafanyika kwa njia ya mtandao katika mfumo wa kwa e-Kilimo kufuata kiungo cha <https://portal.kilimo.go.tz>.

4. Vyama vyote vya msingi vinatakiwa kuzingatia tarehe hizi za ufunguzi wa msimu na kufanya maandalizi muhimu ya kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima mara zinapokuwa tayari. Wito huu unatolewa ili kuondoa ucheleweshaji wa mauzo ya kahawa na malipo kwa wakulima.
5. Bodi ya Kahawa Tanzania itaanza kuendesha minada ya kahawa ghafi katika mkoa wa Kagera (Dry cherry Auction) mara tu itakapopokea taarifa za uwepo wa kiasi cha kutosha cha kahawa kuendesha mnada kutoka kwenye AMCOS. Aidha, Bodi itaanza kuendesha minada ya kahawa safi (Clean Coffee Auction baada ya kupokea taarifa za uwepo wa kahawa na kupokea sampuli kutoka viwanda vya kukoboa kahawa.
6. Vyama vya Ushirika vya Msingi vitapaswa kuhakikisha kuwa akaunti zao za malipo zipo hai (zinafanya kazi) ili kuwezesha zoezi la uuzaji wa kahawa na malipo kufanyika mapema na kuepuka ucheleweshaji wa malipo ya fedha za wakulima.
7. Vyama vya Ushirika vya Msingi vitakavyouza kahawa mnadani vitahuisha vibali vyao au kuomba vibali vipya kwa kujaza fomu maalum. Fomu hizo zinapatikana katika tovuti ya Bodi ya Kahawa, ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa, viwanda vya kukoboa kahawa na ofisi za Vyama Vikuu vya Ushirika. Pale itakapobidi Vyama hivi vitasaidiwa kuomba vibali katika mfumo wa e-Kilimo na maofisa waliopo kwenye ofisi za kanda za Bodi ya Kahawa, Viwanda vya kukoboa kahawa na Vyama Vikuu vya Ushirika.
8. Vyama vya Ushirika vihakikishe kuwa mitambo ya kuchakata kahawa (CPU) iliyoko katika maeneo yao inafanyiwa matengenezo na maandalizi yanafanyika ya kufunguliwa kwa mitambo hiyo mara tu kahawa zinapokuwa tayari. Aidha kila Mtambo unatakiwa kuweka mtunza ubora wa kahawa ambaye atawajibika kusimamia ubora wa kahawa katika kila mtambo. Aidha makampuni yenye nia ya kushirikiana na vyama vya ushirika kuendesha CPU yanatakiwa kuingia makubaliano na vyama husika na kuomba leseni ya kuendesha mitambo ya kuchakata kahawa (Ripe Cherry Processing Licence).
9. Viwanda vyote vya kukoboa kahawa vinatakiwa kuhakikisha kuwa mapokezi yote ya kahawa kutoka kwenye AMCOS na wazalishaji wengine yanaingizwa kwenye mfumo wa UCMS. Utaratibu huu unasisitizwa kwa kuwa taratibu zote za mauzo ya kahawa zitafanyika kwenye mfumo na si vinginevyo.

Imetolewa na:



Primus O. Kimaro

MKURUGENZI MKUU

BODI YA KAHAWA TANZANIA

S. L. P. 732 Moshi, Simu: 027-2752324

Barua pepe: info@coffee.go.tz; Tovuti: www.coffee.go.tz